

**AZIMIO LA BUNGE LA KURIDHIA ITIFAKI YA JUMUIYA YA MAENDELEO  
YA NCHI ZA KUSINI MWA AFRIKA KUHUSU KULINDA HAKIMILIKI ZA  
WAGUNDUZI WA AINA MPYA ZA MBEGU ZA MIMEA  
(THE PROTOCOL FOR PROTECTION OF NEW VARIETIES OF PLANTS (PLANT  
BREEDERS' RIGHTS) IN THE SOUTHERN AFRICAN DEVELOPMENT  
COMMUNITY-SADC)**

---

**KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni miongoni mwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*The Southern African Development Community -SADC*) kwa mujibu wa Mkataba ulioanzisha Jumuiya hii ambao ulisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika mnamo 1992;

**KWA KUWA** Mkataba huu unazitaka Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika kushirikiana kwenye masuala yenye maslahi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi wa nchi hizo;

**KWA KUWA** Ibara ya 22 ya Mkataba wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika wa mwaka 1992 imebainisha umuhimu wa nchi wanachama kuandaa Itifaki zitakazotumika kutoa miongozo ya ushirikiano kwenye masuala yenye maslahi kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa wananchi wa nchi hizo;

**KWA KUWA** Mkataba huo unaelekeza kwamba kila Itifaki itakayoandaliwa itaidhinishwa na mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika na itapaswa kusainiwa na kuridhiwa na Nchi Wanachama;

**KWA KUWA** Katika kutoa mwongozo kuhusu Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya ya Mbegu za Mimea (Protection of New Varieties of Plants) nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini Mwa Afrika ziliandaa Itifaki ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ya Mwezi Mei, 2017 ambayo iliidhinishwa na Mawaziri wa Katiba na Sheria wa Nchi za SADC Mwezi Julai, 2017 na baadae ilithibitishwa na Baraza la Mawaziri wa Kilimo wa SADC mwezi Agosti, 2017.

**KWA KUWA** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organisation- WTO*) kuanzia tarehe 1 Januari, 1995 na kama mwanachama wa WTO inalazimika kutekeleza makubaliano mbalimbali yanayoridhiwa na wanachama wa Shirika hilo na miongoni mwa makubaliano hayo ni kuhusu Makubaliano ya Utekelezaji wa Masuala ya Hakimiliki – *Trade Related Aspect of Intellectual Property Right (TRIPS)*;

**KWA KUWA** Itifaki ya Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (*The Protocol For Protection of New Varieties of Plants (Plant Breeders' Rights) In The Southern African Development Community-SADC*) ilisainiwa Mwezi Agosti, 2018 Jijini Windhoek Namibia Katika Mkutano wa Wakuu wa nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika;

**KWA KUWA** madhumuni ya Itifaki hiyo kama yalivyoainishwa katika Ibara ya 2 ni pamoja na:

- (a) Kuwezesha kuwa na mfumo wa thabiti wa kulinda hakimiliki za wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea;
- (b) Kuhamasisha ugunduzi wa aina mpya za mbegu za mazao ya kilimo; na
- (c) Kutoa Hakimiliki kwa Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea.

**KWA KUWA** Tanzania imasaini, kuridhia na kutekeleza Mikataba mingine inayohusiana na Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea ambayo ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (UPOV-Convention) ambapo Mikataba hii ni muhimu ikatekelezwa kwa pamoja;

**NA KWA KUWA** kuridhiwa kwa Itifaki hii kutakuwa na matokeo chanya yafuatayo:

- (a) Kuweka mfumo wa kulinda Hakimiliki za Wagunduzi wa Mbegu unaokubalika na kutekelezwa katika nchi za SADC na hivyo kuimarisha mahusiano ya nchi yetu na nchi nyingine;
- (b) Hakimiliki itakayotolewa chini ya Itifaki ya SADC itatambulika ndani ya nchi zote wanachama wa SADC, na hivyo kuchochea uwekezaji katika nyanja ya utafiti na ugunduzi wa mbegu mpya wa sekta binafsi;
- (c) Kupanua wigo na kurahisisha biashara ya mbegu na hivyo kuhamasisha ushindani katika tasnia ya mbegu;
- (d) Kuhamasisha na kutoa fursa za utafiti unaolenga kuongeza uzalishaji wa mbegu mpya na hatimaye kuwezesha wakulima kupata mbegu bora;
- (e) Kuongeza upatikanaji wa mbegu bora, kupunguza gharama za usafirishaji na hivyo kupunguza bei ya mbegu kwa mkulima; na
- (f) Kuwezesha upatikanaji wa mbegu zenye ukinzani wa magonjwa, wadudu wa mimea na kuhimili mabadiliko ya tabianchi.

**KWA HIYO BASI**, kwa kuzingatia manufaa yatokanayo na Itifaki hii kwa Tanzania na kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika na pia umuhimu wa kuridhia Itifaki hii, Bunge hili kwa mujibu wa Ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977, linaazimia kuridhia Itifaki ya Hakimiliki za Wagunduzi wa Aina Mpya za Mbegu za Mimea (The Protocol For Protection of New Varieties of Plants (Plant Breeders' Rights) In The Southern African Development Community-SADC) **bila kulazimika kutekeleza masharti ya mkataba ambayo yanaweza kuathiri maslahi ya Taifa.**